
# Mkakati wa Makazi wa NSW: **Mfumo wa Uzoefu wa Kuishi kwa Wakimbizi**

Multicultural NSW inalenga kuwapa watu wenye uzoefu wa kuishi kwa wakimbizi sauti katika maamuzi yanayoathiri maisha yao - hii ni moja ya malengo ya NSW Settlement Strategy (Mkakati wa Makazi wa NSW).

Refugee Lived Experience Framework (Mfumo wa Uzoefu wa Kuishi kwa Wakimbizi) itaongoza Multicultural NSW ili tuweze kujumuisha uzoefu wa kuishi kwa wakimbizi kwa njia zenye maana na kuboresha matokeo ya makazi kwa watu wanaoishi katika NSW.




## Mfumo una sehemu tatu

### 1. Kanuni za Kuongoza

» **Heshima:** Kuthamini uzoefu wa kuishi kwa wakimbizi kama utaalamu na kutambua kila mtu ambaye amechangia.

» **Ushirikiano:** Kufanya kazi pamoja na watu walio na uzoefu wa kuishi kwa wakimbizi kama wabia hai na sawa katika kufanya maamuzi.

» **Usalama:** Kuhakikisha watu wanahisi salama. Hii inajumuisha usalama wa kimwili, kihisia na kitamaduni, kea kuzingatia mahitaji na uzoefu tofauti wa kila mtu.

» **Ujumuishi:** Kutambua kwamba kila mtu ana sifa za kipekee, kusikiliza mitazamo tofauti ya kila mtu, na kuondoa vizuizi vinavyowazuia watu kushiriki.

### 2. Mbinu na Ufundi wa Kukabiliana

Mifano ya vitendo ya jinsi kujihusisha kuzuri kunavyoonekana, pamoja na habari kuhusu:

- **Mazingatio:** Mambo muhimu yanayohitaji kuzingatiwa wakati wa mchakato wa kupanga.
- **Marekebisho:** Njia tofauti za kufanya kazi ili kushinda changamoto.
- **Viwezeshaji:** Sera na desturi zinazosaidia shughuli za ushiriki katika viwango vyote.

### 3. Zana na Rasilimali

Miongozo muhimu na nyenzo zingine za kusaidia kupanga na kuongoza shughuli nzuri za ushiriki.



## Jihusishe

Ili kupata maelezo zaidi kuhusu Mfumo au kujihusisha, skan msimbo wa QR au tembelea https://multicultural.nsw.gov.au/settlement/

Swahili